



**FOMU YA MAOMBI
VITUO ATAMIZI VYA PASS AIC
SUA MOROGORO NA TALIRI KONGWA**



**Kabla ya kujaza fomu, soma maelezo kuhusu sifa za muombaji, masharti ya kuomba
na jinsi ya kujaza fomu, na kuwasilisha fomu iliyopo chini**

- Sifa za Kijana zinazotakiwa: Ueledi wa ujasiriamali, elimu/maarifa, mwenye uzoefu kwenye kilimo na kilimobiashara, awe na tabia njema, utii, nidhamu, mchapa kazi, fikra chanya, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa kike wanapewa kipaumbele.
- Fomu ya maombi inatapatikana kwenye tovuti za AIC (aic.co.tz) na PASS (pass.or.tz), ofisi za PASS, SUA, TALIRI na SUGECO.
- Ada ya fomu ni shs 10,000/-. Ada hiyo ilipwe kwenye akaunti ya PASS, benki ya CRDB.
 - Namba ya Akaunti: 01J1076972802
 - Jina la Akaunti: Private Agricultural Sector Support
 - Tawi: Morogoro
 - Taja jina lako ikifuatiwa na '**Vituo Atamizi PASS AIC**' kwenye kumbukumbu ya malipo (Bank slip); kwa mfano: 'Fatuma James – Vituo Atamizi PASS AIC'
 - Ada hiyo haitarejeshwa hata kama mwombaji hatachaguliwa
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 2/09/2018.
- Mchakato wa maombi utajumuisha: Kujaza fomu, kulipa ada, na kuwasilisha fomu pamoja na kumbukumbu ya malipo kwa PASS AIC.
- Baada ya PASS AIC kupokea fomu; Watachaguliwa vijana 100 kushiriki kwenye mafunzo ya siku 15, ikiwemo siku moja ya kutahiniwa na kuhojiwa. Hatua ya mwisho ya mchakato baada ya mafunzo ni kuchaguliwa kwa vijana 40 watakaoshiriki kwenye vituo atamizi kwa muhula wa 2018.
- Mchakato wa uchaguzi utafanyika Morogoro na kijana atakayeshiriki kwenye mchakato huu na vilevile kwenye vituo atamizi atajikimu kwa gharama zake binafsi.
- Vituo Atamizi kwa muhula wa 2018 ni viwili: SUA Morogoro (uzalishaji wa mbogamboga) na TALIRI Kongwa (unenepeshaji wa mbuzi).
- Fomu za maombi zinapatikana www.aic.co.tz, www.pass.or.tz
- Unaweza kutuma fomu kwa baruapepe kwenda: info@aic.co.tz, au kwa kupeleka kwenye ofisi za PASS iliyopo karibu nawe.



FOMU YA MAOMBI
VITUO ATAMIZI VYA PASS AIC
SUA MOROGORO NA TALIRI KONGWA



1	Jina	
2	Barua pepe	
3	Simu	
4	Anwani	
5	Kijiji / Kata / Mji / Mkoa	
6	Jinsia (Kiume / Kike)	
7	Umri	
8	Hadhi ya Ndoa (chagua moja)	Sijaoa / Nimeoa-olewa / Nimeachika / Mjane / mengineyo
9	Elimu (chagua moja)	Darasa la 7 / Fomu 4 / Fomu 6 / Chuo / Sina elimu
10	Kujua kusoma na kuandika	Ndiyo / Hapana
11	Uzoefu wako juu ya kilimo (Taja; Toa maelezo)	
12	Uzoefu wako juu ya Kilimobiashara (Taja; Toa maelezo)	
13	Shughuli kuu ya kiuchumi unayofanya/jihusisha nayo (chagua unayofanya; toa maelezo ya kina)	Uzalishaji wa mazao / ufugaji / usindikaji / biashara / sina shughuli
14	Kwa nini unataka kujiunga na Vituo Atamizi vya PASS AIC? (Toa maelezo)	